


# Namna Ebola inaenea



## Kutoka ku wanyama wenye ugonjwa

- Ebola inaenea ku watu wakati wanagusa wanyama wagonjwa na majimaji ya mwili yao, kwa mfano:




Kugusa popo, mukojo yao, mavi yao, mate yao, ao kula matunda yenye iliangushwa na popo wenye ugonjwa



Kugusa wanyama wenye ugonjwa



Kula nyama mbichi ao nyama yenye ilikaushwa ku moshi ya wanyama wa pori



## Kutoka ku watu wenye ugonjwa

- Watu **hawawezi** kueneza Ebola mbele waonyeshe dalili.
- Watu wanaeneza Ebola ku watu wengine kupitia majimaji ya mwili wakati wako wagonjwa, kama vile kupitia:



Kugusa jasho, mate, damu, mukojo, mavi, na matapishi



Kugusa watu wagonjwa



Kugusa mwili wa mutu mwenye alikufa



Kuogesha mwili mbele ya kuzika



Kugusa kitu ya mutu mugonjwa ao ya mutu mwenye alikufa



Kufanya ngono na mutu mwenye alikuwa na Ebola hivi karibuni

CDC VITUO VYA AMERIKA VYA KUDHIBITI NA KUZUIA MAGONJWA (U.S. CDC)